

## SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



### **MAFUNZO YA UELEWA JUU YA SUMUKUVU KWENYE MAHINDI NA NAFKA NYINGINE KWA WAFANYABIASHARA AMBAO NI WASAFIRISHAJI NA MAWAKALA WA FORODHA KATIKA MIPAKA YA HOROHORO, HOLILI NA NAMANGA**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuwafahamisha wafanyabiashara ambao ni wasafirishaji na mawakala wa forodha katika mipaka ya Horohoro, Holili na Namanga kuwa limeandaa mafunzo kuhusu sumukuvu kwenye mahindi na nafaka nyingine. Mafunzo haya yatafanyika katika kumbi za mipaka ya Horohoro tarehe **2021-06-07**, Holili tarehe **2021-06-09** na Namanga tarehe **2021-06-10** kuanzia **saa 02:30 asubuhi**.

Mafunzo haya yamelenga kutoa elimu kwa wafanyabiashara ambao ni wasafirishaji na mawakala wa forodha kuhusu sumukuvu na usalama wa mahindi na nafaka nyingine pamoja na taratibu za kufuata katika kusafirisha mahindi na nafaka kwenda nje ya nchi.

Kwa taarifa hii mnaombwa wafanyabiashara ambao ni wasafirishaji na mawakala wa forodha kuhudhuria mafunzo haya muhimu bila kukosa.

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Shirika la Viwango Tanzania,**

**S L P 9524, Dar es Salaam.**

**Simu: +255 (022) 2450298; Hotline: +0800 110 827**

**Barua pepe: [info@tbs.go.tz](mailto:info@tbs.go.tz);**

**Tovuti: [www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)**